

Moyo wangu masikini

Moyo wangu masikini, una ndwele za mapenzi,
Sina tiba asilani, liponacha laazizi,
Penzi langu bila peni, alilonona la kishenzi,
Nateseka masikini, nipayepi wa kupenda?

Nilimweka namba tatu, kwenye watu wa thamani,
Mola mumba nguzo yetu, alishika namba wani,
Mamangu kipenzi chetu, akamfata mwendani,
Nateseka masikini, nipayepi wa kupenda?

Lipojuwa sina changu, akafata mwafulani,
Lijitiya ya ukungu, kuniona mtu duni,
Akavunja moyo wangu, nilompa maishani,
Nateseka masikini, nipayepi wa kupenda?

Leo kwangu penzi tungu, wa kupoza natamani,
Awe ndiye kitu changu, cha thamani maishani,
Tujifunge hata pingu, tulishane na yamini,
Nateseka masikini, nipayepi wa kupenda?

*Ramadhan Abdallah Savonge
"Malenga wa Nchi Kavu",
SEKU, Kitui*